# Sera ya Makato ya CoxHealth

CoxHealth unataka uelewe mchakato wa malipo na makato na rasilimali unazoweka kupata wewe na familia yako.

CoxHealth itatoa huduma za matibabu bila ubaguzi katika hali zote za dharura bila kujali uwezo wa mgonjwa kulipa. Ikiwa una bima kama vile Medicare, Medicaid, bima ya serikali au nyingine ya afya, CoxHealth itaitoza bima yako baada ya wewe kutibiwa. Ikiwa una bima na una maswali kuhusu huduma za bima yako au manufaa unayostahiki, tafadhali wasiliana na kampuni yako ya bima. Ikiwa huna bima na unatimiza masharti fulani ya mapato, unaeza kutuma ombi la kupata Usaidizi wa Kifedha, ikiwa ni pamoja na kupunguzi wa matoto za hospitali na mpango wa kulipa bila riba. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu Sera ya Usaidizi wa Kifedha wa CoxHealth (FAP) na fomu ya kuomba, au kuomba ilani iliyoandikwa au mawasiliano ya kielektroniki kwa kuzungumza na mhudumu wa Huduma kwa Wagonjwa au kwa kupiga simu 417-269-0523. Maelezo na fomu za kuomba zinapatikana katika hospitali au kliniki za CoxHealth au kwenye tovuti www.coxhealth.com.

**Siku ya Huduma**

Katika siku yako ya kuhudumiwa au siku moja kabla, utatakiwa kulipa kiasi kinachikadiriwa kwa ajili ya huduma utakazopokea. Ikiwa una bima, makadirio ya kiasi unachotakiwa kulipa kitategemea manufaa kutokana na bima yako. Ikiwa huna bima, utatakiwa kulipa kiasi cha kuanzia. Ikiwa unapokea matibabu katika Idara ya Matibabu ya Dharuara ya CoxHealth, hutatakiwa kulipa mpaka ufanyiwe ukaguzi wa kimatibabu.

**Taarifa za Bili**

Baada ya kutibiwa, utatumiwa bili za matibabu zikiwa na kiasi tunachokudai. Pamoja na bili yako, tutakutumia maelezo kuhusu jinsi ya kuomba usaidi wa kifedha. Malipo yanatarajiwa ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea taarifa. Ikiwa unahitaji msaada wa kulipa bili yako, kama ungependa kufanya mipango ya kulipia au kama umejumuishwa kupokea msaa wa kifedha, ni muhimu uwasiliane nasi mapema kwa kutupigia simu ukitumia namba za simu zilizo kwenye bili ili akaunti yako isielekezwa kwa shirika la kudai madeni. Unaweza kuomba usaidi wa kifedha hadi siku mia mbili arubaini (240) baada ya siku ya kwanza ya taarifa ya bili yako. Mbali na taarifa za bili, unaweza kupigiwa simu kuhusu akaunti yako.

**Maswali kuhusu bili, Kupinga au Kuomba Bili yenye Ufafanuzi**

Tafadhali wasiliana nasi ukitumia namba ya simu iliyo kwenye taarifa ya bili kama una swali au kama ungependa kupinga bili yako. Unaweza kupata taarifa yenye maelezo ya kipengele kwa kipengele kuhusu matozo kutoka CoxHealth ikiwa utaomba.

**Mipango ya Malipo**

Ikiwa huwezi kulipa kiasi unachodaiwa kikamilifu, unaweza kufanya mpango wa namna ya kulipia bili yako kwa kutupigia simu kupitia namba iliyo kwenye taarifa ya bili. Mipango ya kulipa ni

lazima ukibaliwe pamoja na CoxHealth kulingana na mwongozo ulioorodheshwa hapa chini ili akaunti yako isipelekwe kwa sirika al kudai madeni.   Ikiwa unaamini kwamba huwezi kulipa kiasi kilichoorodheshwa hapa chini, taarifa kamili ya kifedha itatakiwa ili marekebisho yafanywe.

**Mwongozo kwa ajili ya kila hospitali ya CoxHealth**:

| Upeo wa Salio | Lipa kwa Miezi | Kiasi cha Kulipa |
|---|---|---|
| $49 au kidogo | KWA UKAMILIFU | KWA UKAMILIFU |
| $50-$300 | Miezi 3 | $50-$100 |
| $301-$450 | Miezi 5 | $60-$90 |
| $451-$600 | Miezi 6 | $75-$100 |
| $601-$900 | Miezi 7 | $85-$128 |
| $901-$1500 | Miezi 8 | $112-$187 |
| $1501-$3000 | Miezi 12 | $125-$250 |
| $3001-$6000 | Miezi 15 | $200-$400 |
| $6001-9,999 | Miezi 18 | $333 na zaidi |
| Zaidi ya $10,000 | Miezi 24 | $416 na zaidi |

**Mwongozo kwa ajili ya kila Kliniki (Klini ya Ferrell-Duncan, Huduma za Kikanda za CoxHealth, Kliniki za CoxHealth Branson, Kliniki za CoxHealth Monett na Kliniki za Kaunti ya Cox Barton):**

| Upeo wa Salio | Lipa kwa Miezi | Kiasi cha Kulipa |
|---|---|---|
| $49 au kidogo | KWA UKAMILIFU | KWA UKAMILIFU |
| $50-$300 | Miezi 3 | $50-$100 |
| $301-$450 | Miezi 5 | $60-$90 |
| $451-$600 | Miezi 6 | $75-$100 |
| $601-$900 | Miezi 7 | $85-$128 |
| $901-$1500 | Miezi 8 | $112-$187 |
| Zaidi ya $1500 | Miezi 12 | $125 na zaidi |

**Mashirika ya Kudai Madeni**

CoxHealth hutumia mashirika ya kukusanya madeni ili kusaidia katika kukusanya madeni ambayo hayajalipiwa. Ikiwa bili halijalipwa baada ya siku mia moja (120) au zaidi na haipo katika mpango wa kulipia, CoxHealth inaweza kutumia akaunti hiyo kwa mashirika ya kudai madeni ili yakusanye pesa hizo.  Ombi la Usaidizi wa Kifedha litakubaliwa wakati wowote ambapo deni limepelekwa kwa shirika la kukusanya deni.  Mara baada ya agizo kupokelewa, mchakato wa kudai deni utasimamishwa.

Ikiwa deni litakuwa halijalipa baada ya siku mia mbili na atubaini (120), CoxHealth inaweza 1) kuripoti kwa shirika la kuweka kumbukumbu la wakopaji, 2) kufungua shtaka lenye dai dhini ya mgonjwa au 3) pkupiga tanjia mali ya mtu. Kabla ya kuchukua hatua hizi, CoxHealtha itafanya juhudu zinazofaa ili kubaini ikiwa mhusika anastahiki kupata usaidizi chini ya FAP. Siku thelathini (30) kabala ya kuanzisha mchakato wa kudai deni, CoxHealth:

i. Itampa mgonjwa ilani ikiwa na (a) maelezo ya Usaidizi wa Kifedha unaopatikana na wanaostahiki, na (b) itaeleza hatua ambayo CoxHealth inatarajia kuchukua na tarehe ambapo CoxHealth itachukua hatua;
ii. Itatoa nakala ya muhtasari wa FAP kwa lugha rahisi pamoja na taarifa kuhusu jinsi ya kupaya nakala ya ombi la kujiunga na FAP; na
iii. Kuwasiliana na mgonjwa na kutaarifu kwa mdodmo kuhusu kiasi anachodaiwa na uwepo wa FAP.

Tafadhali tahadhari kuwa hatua za kisheria zinaweza kuchukuliwa kwenye mizani yoyote isiyolipwa. CoxHealth haitachukua hatua za kisheria ikiwa chochote chenya punguzo hakijalipwa kwa sababu ya kuidhinishwa kwa ombi la Usaidizi wa Kifedha, ilimradi mapinguzo hayo yawe sahihi na yatumiwe inavyo kutumiwa kwa kila mtu anayestahiki chini ya FAP. Deni lolte linalobaki baada ya mapunguzo hayo, linaweza kuchukuliwa hatua ya kukusanya madeni, ikiwa ni pamoja na hatua za kisheria.

Kabla ya kuripoti kiasi ambacho hakijalipwa kwa shirika la kufuatilia sifa ya wakopaji, kuanzisha shtaka la madai au kupiga tanji mali ya mtu, juhudi zinazostahili zitachukuliwa iki kumfahamisha mtu kuhusu FAP.

CoxHealth haitatoza deni linalobaki baada ya kutumia punguzo la Usaidizi wa Kifedha. Hata hivyo, CoxHealth inaweza, kwa hiari yake pekee, kutoza ushuru kwenye deni ikiwa 1) Mdhamini anapokosa kulipa deni lakeilivyokubaliwa, au 2) salio limepelekwa kwa mashirika ya kudai madeni.

**Usaidizi wa Kifedha**

Tafadhali jisikie huru kuuliza kuhusu Usaidizi wa Kifedha. Tuko tyari kukusidia.

Kuanzia 11/2018